# Ufupisho wa Muhtasari

## Viwango vya Kimataifa kuhusu Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono

Ufupisho huu unayapa mashirika ya kijamii muhtasari wa viwango mbalimbali vya kimataifa kuhusu unyonyaji, dhuluma na unyanyasaji wa kingono (SEAH). Ni muhimu kwa mashirika ya kijamii kufikia viwango husika wakati yanafanya kazi ya maendeleo na kibinadamu ili kulinda wafanyakazi na kutodhuru jamii ambazo unafanya kazi.

### Viwango vya kimataifa na vyombo vya kukabiliana na SEAH

Katika mwaka wa 2018 na 2019 wafadhili wakuu wa kiserikali ambao wanaunda Kamati ya Msaada wa Maendeleo wa OECD waliridhia kwamba kazi yao na ya washiriki wao wote wanapaswa kufuata viwango vya IASC na/au CHS (1-3 vilivyoko hapa chini). Hati ya KCS (nambari 4 hapa chini) ni muhimu hasa kwa mashirika yanayofanya kazi na watoto. Pendekezo la Kamati ya Msaada wa Maendeleo ya mwaka wa 2019 (nambari 5 hapa chini) ni chombo cha kimataifa ambacho kimsingi kilikusudiwa serikali za wafadhili, lakini imejumuishwa hapa ili mashirika yaelewe ni nini wafadhili wamejitolea na viungo kwenye viwango vya IASC na CHS ambavyo vitakuwa vinahusika zaidi.

### 1 Kanuni Sita Kuu za Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali Zinazohusiana na Unyonyaji wa Kingono na Dhuluma

**Je, kwanini kiwango kimewekwa?** Baada ya madai ya SEAH Afrika Magharibi katika mwaka wa 2002 Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali (IASC) ilianzisha Kikosi Kazi kuhusu Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kingono na Dhuluma (PSEA) katika migogoro ya kibinadamu. Kikosi Kazi hicho kilipewa mamlaka ya kuimarisha ulinzi na utunzi kwa wanawake na watoto hasa katika hali za migogoro na mizozo ya kibinadamu, na hasa kutoa mapendekezo yanayolenga kuondoa unyonyaji wa kingono na dhuluma (SEA). Matokeo muhimu yalikuwa ni kanuni sita kuu ambazo huunda kanuni za maadili ya mwenendo wa chini zaidi unaokubalika ambao ulianza kutumika katika Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (ST/SGB/2003/13).

**Je, kiwango hiki kinashughulikia nini?** Kiwango hicho: kinahitaji SEA kutafsiriwa kama utovu mkuu wa nidhamu, pamoja na uwezekano wa kuondolewa kazini; huzuia wafanyakazi kulipia ngono au kubadilishana bidhaa n.k. kwa ngono; huzuia shughuli ya ngono na yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18; huzuia uhusiano wa kinyonyaji na wanaonufaika na au washiriki; hulazimu wafanyakazi kuripoti wasiwasi; na hulazimu wafanyakazi kuunda utamaduni ambao unazuia SEA.

**Je, kiwango hicho kinatumika kwa nani?** Wafanyakazi wote wa Umoja wa Mataifa na yeyote anayefanya kazi kwa ushirikiano wa pamoja/kupokea fedha kutoka kwao. Iwapo unashirikiana na

Umoja wa Mataifa (au mashirika mengine yanayofuata kanuni hizi, kama vile Taasisi za Kimataifa za Fedha, ni lazima ukubali kufuata viwango hivi ili kuzuia SEA .

## 2 Viwango vya Chini zaidi vya Utendaji vya Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali: Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kingono na Dhuluma kwa Wafanyakazi Wenyewe (MOS-PSEA) [1]

**Je, kwanini kiwango hiki kimewekwa?** Kiasilia, kiwango hiki kilibuniwa kusawazisha jinsi Umoja wa Mataifa na yeyote ambaye anapokea fedha za Umoja wa Mataifa analinda wanajamii dhidi ya kukumbana na unyonyaji wa kingono na dhuluma kutoka kwa wafanyakazi wao. Hakishughulikii unyanyasaji wa kingono kwa wafanyakazi ndani ya eneo la kazi. Mashirika mengine, hasa baadhi ya Taasisi kuu za Kimataifa za Fedha, pia hutumia kiwango hiki. Baraza la Kimataifa la Wakala wa Hiari (ICVA), Inter Action na Kamati Tendaji ya Dharura za Kibinadamu (SCHR) wote ni waalikwa wa kudumu katika IASC.

**Je, kiwango hiki kinashughulikia nini?** Kiwango hiki kinahitaji shirika na washiriki wake kuwa na sera iliyowekwa ili kuzuia SEA. Ofisi za kimaeneo na washirika ni lazima waarifu jamii katika eneo husika kuhusu hatua ambazo ofisi yao ya eneo hilo na washirika wanachukua ili kuzuia SEA. Hatua hizi zinajumuisha kuwa na mfumo unaofaa wa kitamaduni kusaidia mtu yeyote kuripoti wasiwasi na kufikia msaada, ikijumuisha wanajamii na wafanyakazi, kuhakikisha hatua za kuajiri zinatambua watu wanaofaa kuajiriwa, na mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu jinsi ya kutekeleza kiwango hicho.

Kiwango hiki pia kinahitaji mashirika kuwa na kituo au idara iliyotengwa kuangazia SEA, kanuni wazi za maadili na kwamba Taarifa ya Katibu Mkuu (ST/SGB/2003/13) au kanuni mtawalia za maadili zinapaswa kujumuishwa katika mikataba.

**Je, kiwango hiki kinatumika kwa nani?** Wafanyakazi wote wa Umoja wa Mataifa na kila mmoja anayefanya kazi na au kupokea fedha kutoka kwao. Iwapo unashirikiana na Umoja wa Mataifa, ni lazima ukubali kufuata viwango hivi ili kuzuia unyonyaji wa kingono na dhuluma. Wafadhili wa Kamati ya Msaada wa Maendeleo wanahitaji kufuatiliwa kwa MOS-PSEA na/au CHS. Hati zote tatu huunda kwa uwazi msingi wa sera wa mapendekezo ya DAC (tazama dokezo la 5 hapa chini).

## 3 Kiwango cha Msingi cha Kibinadamu kuhusu Ubora na Uwajibikaji (CHS)[2]

**Je, kwanini kiwango hiki kimewekwa?** Kiwango hiki hutoa mbinu ya pamoja ya kutoa msaada wa kibinadamu kwa jamii zilizoathiriwa na migogoro. Hii pia inajumuisha jinsi ya kuzuia na kuitikia SEAH, sawia na mahitaji ya MOS PSEA. Ahadi mbalimbali ndani ya Kiwango cha Msingi cha Kibinadamu, ikiwa zitafikiwa, pia zitachangia kuunda mashirika salama zaidi.

**Je, kiwango hiki kinashughulikia nini?** Kiwango hiki kinahitaji hatari za SEAH kutambuliwa na kushughulikiwa ndani ya mashirika na shughuli za programu zao. Mashirika ni lazima yaweke sera ili kuzuia na kuitikia SEAH. Jamii ni lazima zijulishwe kuhusu kazi ya shirika katika kuzuia SEAH. Mifumo ya kuripoti ni lazima iwepo kwa ajili ya jamii kutoa ripoti. Michakato ya kuripoti na uchunguzi ni lazima ipatie usalama, mahitaji na maslahi ya waathiriwa na manusura kipaumbele.

1 https://interagencystandingcommittee.org/system/files/3_minimum_operating_standards_mos-psea.pdf
2 https://corehumanitarianstandard.org/the-standard

A[Kielelezo cha CHS PSEAH kilichapishwa katika mwaka wa 2020 ], wakati unyanyasaji wa kingono ulijumuishwa kwa mara ya kwanza.

**Je, kiwango hicho kinatumika kwa nani?** Kiwango hiki kiliandikwa kwa ajili ya kazi ya kibinadamu lakini Muungano wa CHS hutetea kwamba kila mmoja anayetoa kazi ya maendeleo anaweza kutumia.

### 4 Viwango vya Kimataifa vya Kulinda Usalama wa Watoto kwa Kuweka Watoto wakiwa Salama [3]

**Je, kwanini kiwango hiki kimewekwa?** Kulinda watoto kutokana na aina zote za ukatili na dhuluma, ikijumuisha SEA kwa watoto ambazo zinaweza kuibuka kutokana na msaada wa kibinadamu au kimaendeleo unaotolewa.

**Je, kiwango hiki kinashughulikia nini?** Kiwango hiki kinahitaji mashirika yote yanayokaribia watoto kuwa na sera ya kulinda usalama wa watoto. Kiwango hiki kinahakikisha kila mmoja anayefanya kazi na watoto anapewa mafunzo na msaada ili kulinda usalama wa watoto. Mashirika ni lazima yajumuishe hatua za kulinda usalama wa watoto katika shughuli na michakato yote ya shirika. Mifumo ya kuripoti ni lazima iwe inapatikana kwa kila mmoja ambaye angependa kuripoti wasiwasi, hasa watoto.

**Je, kiwango hicho kinatumika kwa nani?** Viwango hivi vinatumika kwa hiari ya shirika lolote lakini vinahusika hasa kwa mashirika ambayo kazi yake inahusisha, au kuathiri watoto.

### 5 Pendekezo la Kamati ya Msaada wa Maendeleo 2019[4] kuhusu Kumaliza Unyonyaji, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono katika Ushirikiano wa Maendeleo na Msaada wa Kibinadamu[5]

**Je, ni kwanini hati hii ipo?** Serikali ambazo hutoa fedha kwa ajili ya maendeleo na kazi za kibinadamu zilitaka kutoa kiwango katika kazi yao ili kuzuia na kuitikia SEAH.

**Je, hati hii inashughulikia nini?** Inatoa kipaumbele kwa haki, mahitaji na maslahi ya waathiriwa na manusura wa SEAH. Mashirika ambayo hupokea fedha ni lazima yawe na sera na kanuni za maadili ambazo zinashughulikia SEAH. Mifumo ya kuripoti ya siri na inayoficha anayeripoti ni lazima iwe inapatikana kwa kila mmoja ambaye anataka kutoa ripoti. Hii inajumuisha wafanyakazi na wanajamii. Mashirika yanapaswa kuweka kumbukumbu za hatua za kulinda usalama ambazo wanatekeleza. Hii inawasaidia katika kufuatilia mafanikio yao na kufikiri kuhusu kile wanapaswa kuboresha.

Hati hiyo pekee inatambua "*Kanuni na Viwango vya Chini zaidi vya Uendeshaji vya Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali kuhusu Kuzuia Unyonyaji wa Kingono na Dhuluma (MOS-PSEA), na Kiwango cha Msingi cha Kibinadamu cha Ubora na Uwajibikaji (CHS), kama viwango muhimu*

3 https://www.keepingchildrensafe.global/wp-content/uploads/2020/02/KCS-CS-Standards-ENG-200218.pdf
4 Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo (OECD) ni shirika la kimataifa ambalo linafanya kazi na serikali, watunga sera na wananchi ili kukuza sera na viwango vya kimataifa ambavyo vinakuza usawa na fursa kwa wote. Shirika la OECD lina Kamati ya Msaada wa Maendeleo ambayo huwaleta pamoja baadhi watoaji msaada wa maendeleo wakubwa duniani ili kufuatilia jinsi fedha zinatumika, kukuza viwango na kufuatilia kazi ya wanachama katika msaada wa maendeleo. Kwa sasa kuna wanachama 30 wa DAC. https://www.oecd.org/dac/development-assistance-committee/
5 http://www.oecd.org/officialdocuments/publicdisplaydocumentpdf/?cote=DCD/DAC(2019)31/FINAL&docLanguage=En

*vya kimataifa"*. Hivyo kwa hiyo, Pendekezo la DAC haliundi kiwango kipya, ila linaangazia matumizi ya viwango vya IASC na CHS kwa wafadhili.

**Je, hati hii inashughulika na nani?** Serikali ambazo ni wanachama wa Kamati ya Msaada wa Maendeleo na shirika lolote linalofanya kazi na wao wanapaswa kuhakikisha kazi yao ya kukabiliana na SEAH inaongozwa na hati hii. Serikali na mashirika ambayo si wanachama wa Kamati ya Msaada wa Maendeleo pia wanahimizwa 'kufuata' hati hii na mashirika kadhaa ya Umoja wa Mataifa yamefanya hivyo.

Ili kutumia viwango hivi na vyombo vya kimataifa vilivyotajwa hapo juu, rejelea Dokezo la RSH la Jinsi ya kutumia viwango vya sekta ya SEAH.